

## Maswali na Majibu

1. Mungu alionyesha upendo wake kwa Adamu na Hawa namna gani?  
*Mungu aliwapa bustani ya Edeni, chakula kingi na kazi nzuri.*
2. Mbona Mungu alijaribu Adamu na Hawa? *Kuona kama wanampenda na watamtii*
3. Jaribio lilikuwa gani? *Wasile tunda la mti wa ujuzi wa mema na maovu.*
4. Adamu na Hawa waliitikiaje kwa hilo jaribio?  
*Hawa alisikiliza nyoka na akakula hilo tunda, Adamu naye alikula.*
5. Mbona tusimlaumu mtu mwingine kwa sababu ya dhambi zetu?  
*Sisi wote tunatakiwa tuajibikie dhambi zetu.*
6. Adhabu kuu ya dhambi ilikuwa ni gani?  
*Kifo. Mungu anatoa pumzi yake ya uhai na mwili unarudi kwa mchanga.*
7. Hiyo adhabu inatuadhiri namna gani?  
*Kila mtu ametenda dhambi kwa hivyo kila mtu anakufa.*
8. Adhabu zingine zilikuwa gani?  
*Nyoka aende kwa tumbo, Hawa apate watoto kwa uchungu na Adamu afanye kazi ngumu ili apate chakula*
9. Mungu aliacha Adamu na Hawa bila tumaini?  
*Hapana. Mungu aliwahidi uzima na hiyo iliwapa tumaini.*
10. Mungu aliahidi Adamu na Hawa nini?  
*Katika Yesu, dhambi zetu zinasamehewa na tunapata uzima*
11. Mbona Kaini alikasirikia Habili na Mungu.  
*Mungu hakukubali sadaka yake, lakini akakubali ya Habili.*
12. Mbona tutawale dhambi?  
*Dhambi moja huwa inasababisha nyingine kwa hivyo tusipoishinda itatutawala.*

**Mistari ya kukariri** Mwanzo 3:15 na Mwanzo 3:19

**Mazungumzo** Kuna uhusiano gani kati ya Mwanzo 3:15 na Warumi 6:23?

**Kuandika Umejifunza nini juu ya dhambi.** Andika juu:

- mwanzo wa dhambi
- adhabu ya dhambi
- kuokoka kutoka kwa dhambi

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



## Somo la 3 Bustani ya Edeni

**SOMA** Mwanzo mlango wa 3 na 4

### SOMO

**Mungu alipenda Adamu na Hawa** sana na akawapa kila kitu ili awafurahishe. Aliwatengezea bustani nzuri sana ya kuishi. Kulikuwa na miti mingi na mimea iliyozaa matunda mengi ya Adamu na Hawa wakule. Kazi ya Adamu ilikuwa kutunza hiyo bustani ya Edeni. Ilikuwa kazi rahisi kwa sababu ilimea yenyewe na hakukuwa na makwekwe.

**Mungu alitaka kujua kama Adamu na Hawa wanampenda:** Mungu aliamua kujaribu Adamu na Hawa ili aone kama watamtii. Haikukuwa jaribio gumu. Katikati ya bustani kulikuwa na mti ulioitwa mti wa ujuzi wa mema na maovu. Mungu aliwambia lazima wasikule tunda la huo mti. Wakikula watakuwa wameasi Mungu – watakuwa wamefanya dhambi. Ni muhimu sana kutii amri za Mungu. Ilikuwa ya maana kwa sababu Mungu alikuwa amemwambia Adamu kwamba wakimuasi, watakufa.



**Nyoka alimjaribu Hawa ili aasi:** Alimwambia kwamba hatakufa akila tunda kutoka kwa huo mti; atakuwa na akili kama Mungu. Hawa alikula lile tunda. Alimpa Adamu naye pia hilo tunda na akala. Papo hapo wakajua wamefanya makosa. Wakajua wako uchi na wakaibika. Wakatengeneza mavazi kutoka kwa majani ya mtini.

Mungu alikuja kwa bustani ili azungumze na Adamu na Hawa. Mungu aliuliza Adamu kama amekula hilo tunda. Adamu alilaumu Hawa; alimwambia kwamba ndiye alimpa tunda na akala. Hawa alilaumu nyoka. Ni rahisi kulaumu wengine wakati tumefanya makosa lakini ni juu yetu kujua dhambi nini. Nyoka alimwambia uongo, lakini uamuzi wa kukula ulikuwa wa Adamu na Hawa. Ilikuwa juu yao kujua wanafanya dhambi. Mungu aliwaadhibu wote.

**Mungu anawaadhibu:** Adhabu kubwa kwa Adamu na Hawa ilikuwa kifo. Walianza kukua wazee na mwishowe walikufa. Mungu aliumba Adamu kutoka kwa mchanga.

Alimpulizia pumzi ya uhai kwa mapua. Adamu akawa hai (Mwanzo 2:7). Sasa Adamu na Hawa wamefanya dhambi. Mungu alikuwa amesema adhabu ya dhambi (kufanya makosa) ni kifo. Mungu alisema Adamu na Hawa kukufa, ni kutoa pumzi ya uhai ndani yao. Halafu miili yao itarudi chini kwa mchanga (Mwanzo 3:19).

Kifo ni adhabu ya kila mtu anayefanya dhambi. Sisi wote hufanya dhambi katika maisha yetu. Kwa hivyo adhabu yetu ni kifo. Tukifa, Mungu hututoa pumzi inayotuweka hai. Tunazikwa chini kwa hivyo miili yetu hurudi mchangani. Tunaacha kuishi.

Adhabu zilikuwa;

- Nyoka atembelee tumbo
- Hawa atii mumewe tena azae watoto kwa uchungu.
- Adamu afanye kazi kwa bidii ili akuze chakula kwa sababu sasa makwekwe yatakua.

**Ahadi ya tumaini:** Mungu alipenda Adamu na Hawa, ingawaje walikuwa wamefanya makosa. Mungu alitaka wawe na tumaini. Alifanya ahadi na Adamu na Hawa alipoadhibu nyoka. Mungu alisema, “Nitaweka uadui kati yako na mwanamke, kati ya uzao wako na wake; ataponda kichwa chako na utaponda kisigino chake.”

Hii ahadi ni ya maana sana kwa sababu ndiyo ilikuwa ahadi ya kwanza kwa mwanadamu. Ni ngumu kidogo kuelewa, kwa hivyo tutaingalia kwa kindani. Neno ‘uadui’ linamaanisha chuki. ‘Uzao’ linamaanisha kizazi. Kumbuka kwamba Mungu alikuwa anaambia nyoka. Maneno yaliyofungwa hapo chini yanaonyesha Mungu alikuwa anaambia nani. Na maneno yaliyoandikwa kwa kitaliki yanaeleza maana yake.

- Mimi (Mungu) nimeweka uadui kati yako (nyoka) na mwanamke.  
*Nyoka alimdanganya mwanamke akafanya dhambi kwa hivyo hiyo ni dhambi. Watu wajaribu kuheba dhambi.*
- Na katika uzao wako ( wa nyoka) na uzao wake ( wa mwanamke):  
*Uzao wa mwanamke ni Yesu. Baba yake ni Mungu. Yesu hakukuwa na baba mwanadamu, ingawaje alikuwa na mama wa kibinadamu, Mariamu. Nyoka ni mfano wa dhambi. Hii ina maana Yesu alikuja kuharibu dhambi.*
- Yeye (Yesu) ataponda kichwa chake (nyoka): *Kuponda kichwa ni kuua. Nyoka ni mfano wa dhambi. Hii ina maana kwamba Yesu aliharibu dhambi. Yesu hakutenda dhambi Lakini alipewa njia ya kuharibu dhambi kabisa.*
- Na wewe (nyoka) utaponda kisigino chake (Yesu): *Kuponda kisigino cha mtu ni uchungu sana na inaweka kidonda kwa muda. Hii ina maana dhambi Iliumiza Yesu. Yesu alikufa kifo cha uchungu msalabani. Lakini hakukaa mautini ndani ya kaburi. Ilikuwa kwa muda mchache tu. Baada ya siku 3, alikuwa hai tena.*

Soma Warumi 6:23. Kila mtu hufanya dhambi kwa sababu anakufa. Mungu alipea Adamu na Hawa ahadi kwamba siku moja dhambi na kifo vitaharibiwa. Mwanadamu alipewa tumaini la uzima wa milele.

**Damu inamwagwa ili dhambi ifunikwe:** Mungu alitengeneza Adamu na Hawa mavazi kutoka kwa ngozi ili iwafunike. Mnyama aliuawa ili mavazi yatoke ya kuwafunika. Hili lilikuwa ni somo la kuwasaidia wajue kwamba damu inamwagwa ili dhambi ifunikwe au isamehewe. Hii ilitazamia wakati Yesu angezaliwa afe na amwage damu ili dhambi za waumini zisamehewe. Tangu wakati wazamani, watu walileta sadaka za wanyama kwa kumwaga damu ili Mungu awasamehe. (Waebrania 9:22)

Adamu na Hawa walilazimishwa kuondoka kwenye bustani ya Edeni kwenye kuna mti wa uzima. Waliishi maisha magumu mpaka walipokufa.

**Kaini na Habili:** Hawa alimzaa Kaini tena akamzaa Habili. Kaini alipokua mkubwa alikuwa mkulima wa mboga, lakini Habili alikuwa mfugaji wa kondoo. Walipokuja kumtolea Mungu sadaka, Kaini alileta baadhi ya mboga alizopanda na Habili alileta mmoja wa kondoo wake. Mungu alikubali toleo la Habili kwa sababu alimtolea mnyama vile alikuwa amesema. Kaini hakumsikia Mungu na kumtii. Kaini alikasirika sana kwa sababu Mungu hakukubali toleo yake.



**Dhambi ilitawala:** Mungu alimwambia Kaini na kumwelezea kwamba ni lazima atii Mungu akitaka amkubali. Mungu alimwaadharisha Kaini kwamba anatakiwa asikubali dhambi imtawale - aishinde dhambi. Kaini hakusikiliza Mungu. Alikaa na hasira. Alikuwa na wivu na kumkasirikia nduguye Habili. Kaini alikosa tena. Kaini alienda uwandani na Habili na akamuia kule. Sasa Kaini alifanya makosa mawili.

Mungu alimzungumzia Kaini na akamuuliza, “Wapi ndugu yako?” Kaini alijibu kwa uongo. “Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” Sasa Kaini alifanya makosa matatu.

Dhambi zilifuatana. Mungu alijua kwamba dhambi ilitawala Kaini kwa hivyo alimfukuza. Kama Kaini angesikiliza Mungu na akashinda shida ya kwanza, hangeweza kufanya makosa mengine. Ni lazima tusitawaliwe na dhambi. Tusikubali dhambi moja ituelekeze kwa zingine. Tukiendelea kutenda dhambi, itatutawala.